

# Mfumo jumuishi wa Jinsia Zote na Nadharia

Mwongozo wa Kugeuza Nadharia kuwa Vitendo



United States Institute of Peace
Making Peace Possible

**MWONGOZO HUU ULIANDIKWA NA KATHLEEN KUEHNAST NA DANIELLE ROBERTSON.**

Timu ya muongozo imefaidika sana kwa maoni ya wafanyakazi wenzetu wa USIP: David Connolly, Joseph Hewitt, Illana Lancaster, Alison Milofsky, Steve Steiner, Rosarie Tucci, na Michael Zanchelli. Zaidi ya hayo, timu ilishukuru sana mwongozo kutoka kwa Sanam Anderlini (International Civil Society Action Network), Gary Barker (Promundo-US), na Pamina Firchow (Chuo Kikuu cha George Mason) katika mchakato wote. Shukrani maalum kwa Luba Lukova kwa sanaa nzuri na Chris Brown kwa kazi yake ya michoro. Timu inamshukuru pia Hashim Pondeza kwa kutafsiri muongozo huu kwa Kiswahili.

Maoni yaliyotolewa katika mwongozo huu ni maoni binafsi ya waandishi pekee. Hayawakilishi maoni ya Taasisi ya United States Institute of Peace. Toleo la ripoti hii na nyingine zinazohusiana nayo zinaweza kupatikana katika tovuti yetu (www.usip.org), pamoja na taarifa zaidi kuhusu mada hii.

© 2018 by the United States Institute of Peace

**UNITED STATES INSTITUTE OF PEACE**
2301 Constitution Avenue NW
Washington, DC 20037

Simu: 202.457.1700
Faksi: 202.429.6063
Barua pepe: usip_requests@usip.org
Tovuti: www.usip.org

ISBN: 978-1-60127-732-9

United States Institute of Peace
Making Peace Possible

# Mfumo jumuishi wa Jinsia Zote na Nadharia

## Mwongozo wa Kugeuza Nadharia kuwa Vitendo

Utangulizi: Kubuni Miradi jumuishi ya Jinsia Zote . . . . 2

Mgogoro wa Vurugu Hubadilisha Vipi Kanuni za Kijinsia? . . . . 4

Nini Hufanyika Wakati Miradi Inapopuuza Mienendo ya Kijinsia? . . . . 7

Njia Tatu za Uchambuzi wa Jinsia . . . . 9

Njia ya Wanawake, Amani na Usalama . . . . 10

Njia ya Kiume yenye Amani . . . . 12

Njia ya Utambulisho Inayoingiliana . . . . 14

Kuendelea Mbele na Uchambuzi Wa Jinsia . . . . 16

# Utangulizi: Kubuni Miradi jumuishi ya Jinsia Zote

Mgogoro wa vurugu inavuruga na mara nyingi huzigawa jamii—huharibu miundo ya kijamii, hususan katika majukumu na uhusiano kati ya wanaume na wanawake. Katika mazingira hatarishi na yaliyoathiriwa na migogoro, wajengaji wa amani ni sharti wazitatue athari zinazosababisha migogoro ya jamii zilizogawanyika kwa vurugu. Ongezeko la kuingiza vijana katika vikundi vya kijeshi haramu ni chanzo kimojawapo, na vurugu za kijinsia zinazoenea huathiri watu wote katika jamii, hata baada ya vurugu kumalizika. Hata hivyo, uchambuzi wa kijinsia hautiwi maanani au kujumuishwa sana katika uundaji wa mradi wa kuzuia na jitihada za kupunguza migogoro. Kuanzisha mradi jumuishi wa jinsia zote ni muhimu katika kuunda njia bora za kuzuia mgogoro wa vurugu na kudumisha amani—sio jambo lisilo muhimu na halipaswi kuwazwa baadaye.[1] Nadharia na Mfumo wa Kujumuisha Jinsia Zote (GIFT) ni njia rahisi lakini ya kina ya kuanza kujumuisha uchambuzi wa kijinsia katika uundaji wa miradi.

Njia hii ya kwenda juu inaambatana na njia za ufuatiliaji na kutathmini—uchambuzi wa kijinsia unapaswa kujumuishwa ndani ya mradi. Kufanya uchambuzi wa kijinsia wakati wa hatua ya kubuni miradi, kutawezesha wasimamizi wa miradi kuzingatia vyema athari za migogoro ya kijinsia. Pia kutawezesha miradi iwe imara zaidi kukabiliana na matatizo ya kijamii na kitaasisi wakati wa utekelezaji kwa sababu kazi hii itakuwa tayari imeambatana na kukubaliana na hali mbalimbali za kijamii.

## GIFT

- Elezea jinsia;
- Eleza uhusiano kati ya jinsia na hali ya vurugu na umuhimu wake katika kujenga amani;
- Ichunguze nadharia ya mabadiliko na mfumo wa uchambuzi wa kujumuisha jinsia zote na
- Toa mwongozo maalum kuhusu kujumuisha jinsia katika muundo wa mradi.



## Mwongozo Huu ni wa Nani?

Kifaa hichi cha marejeo ya haraka ni cha wasimamizi wa miradi ambao wangependa kujumuisha mchakato wa kijinsia ndani ya kazi zao—iwe ni wataalam au sio wataalam wa maswala ya kijinsia. Mwongozo huu unawapa wasimamizi wa miradi maswali ya moja kwa moja ili kuanza mchakato. Mchakato wa kijinsia unaweza kuboresha muundo wowote wa mradi—kuanzia ile inayozingatia kuboresha hali ya kijinisa hadi kwa ile zinazozingatia kubadilisha mifumo ya utawala—kwa sababu inalenga ukosefu wa usawa wa mamlaka na fursa ya kubadilisha mifumo. Mwongozo utasaidia 1) kuchunguza dhana kuhusu jinsia wakati wa awamu ya kubuni, 2) kuchambua hoja wakati wa utekelezaji, na 3) kuhakikisha maoni jumuishi yamekusanywa wakati wa kutathmini. Ingawa mwongozo huu umeundwa maalum kwa kazi za kudumisha amani, sehemu kubwa ya dhana zake ni muhimu sana kwa tasnia ya ustawi kiujumla na miradi mingine katika mazingira hatarishi.

# Je, Mgogoro wa Vurugu Unabadilishaje Maadili ya Kijinsia?

Mgogoro ni hali ya kawaida katika jamii ya binadamu. Lakini wakati mgogoro ukigeuka kuwa vurugu, unaweza kusambaratisha jamii au nchi. Hili linapofanyika, vurugu hubadilisha maadili kwa haraka, tabia na matarajio ya washirika wa jamii na mara nyingi kubadilisha majukumu ya wanaume na wanawake wakati wa vurugu na hata baadaye. Mgogoro wa vurugu mara nyingine huwapa wanawake nafasi mpya katika jamii[2]. Wanaume wanapoacha nafasi za kazi au wakijeruhiwa au kuuawa, wanawake wanaweza kushiriki katika majukumu zaidi ya umma, kisiasa au kiuchumi. Lakini vurugu pia inaweza kubana majukumu na matarajio ya wanawake na wasichana, na kutoimakinikia huwapa wengine nafasi ya kuwadhibiti wanawake na wasichana. Kwa mfano, vikundi vya vurugu vya msimamo mkali kama ISIS vimeweka kanuni za kijinsia kuzuia zaidi mienendo ya wanawake na wasichana na adhabu kali ikiwa zitakiukwa.

Wanaume, wanawake, wasichana na wavulana huwa na uzoefu tofauti wa mgogoro na vurugu, kama mashahidi, waathiriwa na watekelezaji. Wakati vurugu ikibadilisha jamii, hata imani kuhusu tabia tarajiwa ya wanawake na wanaume hubadilika pia. Itikadi, maadili na matarajio ya wanawake, wanaume, wavulana, wasichana na makundi madogo ya kijinsia na kingono ni "mtazamo wa kijinsia."[3]

## Kufafanua Jinsia na Mitazamo ya Kijinsia

Jinsia inafafanuliwa vyema zaidi kama kanuni ya mipango inayobadilika katika jamii. Ni zaidi ya hali ya mtu jinsia ya kimaumbile (Mwanaume/mwanamke) Jinsia ni muundo wa tabia za kujifunza ambazo hujumuishwa katika kila kitu tunachofanya kibinafsi, kijamii na kitaasisi. Mtazamo wa kijinsia ni ujamii na kukubali majukumu na matarajio ambayo jamii huona kuwa ni muhimu zaidi kwa mtu—wanaume, wanawake, wasichana, wavulana na vikundi vidogo vya kingono na kijinsia. Mtazamo wa kijinsia wa mtu unaweza kubadilika wakati wa mabadiliko ya jamii kulingana na maadili, desturi na matarajio mapya



Katika awamu za kwanza za kupanga mradi wowote, uchambuzi wa kijinsia unaweza kufafanua sehemu zaidi za kuingilia kati, vyanzo vya uhasama na visababishi vya mgogoro. Uchambuzi wa kijinsia utafafanua kwa muktadha mkubwa wa mradi, licha ya madhumuni au malengo yake. Uchambuzi wa kijinsia utahakikisha angalau utekelezaji wa mtazamo wa “kutofanya madhara”.

Ukosefu wa usawa wa kijinsia na kiutawala unaweza kuwa sababu za kuenea umasikini wa hali ya juu, ukosefu wa chakula, afya dhaifu, vurugu dhidi ya wanawake, na mgogoro wenyewe wa vurugu.[4] Wakati njia za kukabiliana na udumishaji amani zinazingatia jinsia, zitasaidia kupunguza vurugu za kijinisa, kuimarisha usawa wa kijinsia, kupunguza mgogoro, na kuwezesha kuwa na amani ya kudumu. Mradi utajaribu kuimarisha sekta ya usalama katika jamii fulani, kwa mfano, lakini unapaswa kuundwa kwa kuelewa uhusiano tofauti walionao wanaume, wanawake, wavulana na wasichana kwa polisi au vikosi vya usalama. Mpangilio bora wa mradi unapaswa kuambatana na hali ya kijinsia.

## Je, Kugeuza Nadharia kuwa Vitendo ni nini?

Kila kifungu kinajumuisha maswali ya mwongozo na pia kifungu cha "kugeuza nadharia kuwa vitendo." Vifungu hivi vinasaidia kuweka dhana ieleweke vyema kwa kuchunguza aina ya maswali utakayouliza wakati wa kufanya uchambuzi wa jinsia jumuishi katika mradi wa utawala nchini Nigeria, kwa mfano. Vifungu hutoa muktadha mfupi na halafu hupendekeza njia zaidi za uchunguzi ambazo mradi unaweza kujiunga ndani ya muundo wake wakati mabadiliko ya kijinsia yanaangaziwa.

## Maswali ya Mwongozo:

- Ni kwa kiasi gani majukumu na tabia, za wanaume na wanawake, wote wakubwa kwa wadogo, zimebadilika katika harakati ya kukabiliana na mgogoro?
- Je, ni aina gani za vurugu zinatendeka? Je, zinaathiri wanaume na wanawake kwa njia sawa au tofauti?
- Je, maisha na upataji elimu, ajira na mapato umebadilika? Kama ni hivyo, wanaume na wanawake wameathirika kwa njia zipi hasa?
- Je, kuna ukosefu wa usalama wa aina gani? Ukosefu huu wa usalama unaathiri vipi familia, jamii na serikali?
- Je, upatikanaji wa nafasi za kisiasa, kiuchumi na maendeleo ya kijamii kwa wanaume na wanawake unafanana zaidi au kidogo kutokana na vurugu? Kama sivyo, ni maswala gani tofauti yanayowaathiri wanaume na wanawake, wasichana na wavulana?
- Utaelezeaje dhana ya kijinsia ya kwa kikundi au jamii iliyokusudiwa?

## Kugeuza Nadharia kuwa Vitendo: Afghanistani

Historia ya Afghanistani imekumbwa na uchumi wenye misukosuko na mazingira ya ukosefu wa usalama. Licha ya jitihada za kuimarisha mfumo rasmi wa kisheria, takribani asilimia 80 ya migogoro hutatuliwa kupitia mifumo isiyo rasmi. Wakati wa kuunda mradi wa kuimarisha utawala wa Sheria Afghanistani, ni muhimu sana kuelewa uwezo tofauti wa ufikiaji na hadhi za wanaume na wanawake ndani ya mitindo ya kusuluhisha migogoro kijamii . Kwa mfano, ni kina nani wanaofanya uamuzi katika mifumo hii? Je, wanawake wanawakilishwa na mawakili, chifu, au mahakimu ili kuwezesha michakato hii? Tukiangazia maswali kuhusu ufikiaji na upeanaji haki kwa wanaume na wanawake—katika muktadha wa sasa na wa kihistoria—kunaweza kuanzisha nafasi mpya za kazi zinazolenga mahitaji ya wanawake na wasichana. Kazi nyingine inaweza kujumuisha kuelimisha wanaume juu ya umuhimu wa upatikanaji wa haki kwa wanawake na wasichana na mchango wao katika kuunda mifumo ya haki na kutatua migogoro.

# Je, Nini Hufanyika Wakati Miradi Inapopuuza Mabadiliko ya Jinsia?

Uchunguzaji uhusiano kati ya mgogoro, utawala, na jinsia kunatoa ufahamu zaidi kuhusu vyanzo vya msukosuko na nafasi za kudumisha amani ambayo la sivyo inaweza kupotea. Migogoro au vita vina uwezo mkubwa wa kupunguza usawa, kupunguza maendeleo ya wanawake na wasichana, na kuwaweka katika hatari kubwa ya vurugu za kijinsia.[5] Mgogoro wa vurugu pia unaweza kupunguza majukumu ya wanaume katika jamii, na kuwaacha na ufahamu mdogo wa kiutu uzima wakihisi kuwa wanaume ni watu wa vurugu, ambapo vurugu huwa ndio njia msingi ya kutatua matatizo.

## Muundo Shirikishi

Ingawa mwongozo huu unapaswa kutumiwa na wasimamizi wa miradi, maswali ya mwongozo yaliyotolewa yanaweza pia kujumuishwa katika muundo shirikishi au mafunzo yenyewe. Kushughulisha washikadau katika majadiliano kuhusu haya maswali kunaweza kufafanua mabadiliko ya kijinsia na kuondoa maoni potovu.

## Kugeuza Nadharia kuwa Vitendo: Misri

Baada ya mgogoro wa vurugu, uchaguzi unaweza kuashiria ubadilishwaji wa utawala kutoka serikali moja hadi nyingine kwa mtazamo wa amani. Lakini, tafiti zinaonyesha kwamba wapiga kura wanawake wanapitia migogoro mara nne zaidi ukilinganisha na wanaume, na mashambulizi hufanyika wakati wa usajili wa wapiga kura, katika vituo vya kupigia kura, au katika shughuli zingine za kijamii.[6] Wanawake wanalengwa kama wapiga kura, wagombeaji, maafisa wa uchaguzi, watetezi wa haki au viongozi wa vyama vya kisiasa. Wakati wa uchaguzi wa mwaka 2011 nchini Misri, baadhi ya wanawake walitishiwa kupewa talaka kama wasingepiga kura kama ambavyo waume zao walivyosisitiza.[7] Miradi ambayo inakosa kuangazia hatari maalum ambazo wanawake na wasichana wanakumbana nazo katika mfumo wa kisiasa inadhoofisha mchakato wa kidemokrasia na basi kuzuia ushirika wa kiadilifu wa wanawake katika siasa. Aina hizi za vitisho vinaonyesha kutokuwa na usalama katika jamii.



## Kugeuza Nadharia kuwa Vitendo: Sudan Kusini

Hali za kijinsia hazibadilishwi tu na mgogoro lakini pia zinaweza kuchochea mgogoro. Vita katili vya Sudan Kusini vilianza Disemba 2013, na uchambuzi mwingi umelenga kwenye sababu za kisiasa. Lakini, utafiti mpya unahusisha moja kwa moja suala la gharama ya mahari—ambapo mali za familia ya bwana arusi zinaenda kwa familia ya bibi arusi—kwenye mgogoro wa vurugu.[8] Bei ya juu sana ya mahari inaweza kuzuia mfumo wa ndoa na kwa hivyo kuongeza uwezekano wa mgogoro wa vurugu. Kwa mfano, kujiunga na vikundi vya wanamgambo au kutekeleza uvamizi wa kinguvu vurugu wa ng'ombe kunaweza kusaidia wanaume kupata mali wanazohitaji kulipia mahari. Ikiwa mradi wa kudumisha amani katika Sudan Kusini unashughulikia maswala ya kisiasa au utawala pekee na kupuuza hali ya jinsia, vurugu za kila siku kama wizi wa ng'ombe utapuuzwa na kuendelea kuwa pigo kwa jamii.

## Kwa nini Uchambuzi wa Kijinsia ni muhimu kwa Miradi?

Uchambuzi wa vurugu kwa kawaida hukagua miundo, washiriki, na mabadiliko ya muktadha wa vurugu ili kuelewa vizuri zaidi vyanzo vya msukosuko. Uchambuzi wa kijinsia wa vurugu hufafanua uhusiano wa utawala kati ya wanaume, wanawake, wasichana, wavulana, na utambulisho mwingine wa kijinsia katika jamii inayopitia mgogoro wa vurugu, ikiwemo kufikia na kudhibiti rasilimali na kuchangia katika kufanya uamuzi ndani ya sekta kadhaa.

# Njia Tatu za Uchambuzi wa Kijinsia

Uchambuzi wa kijinsia unapaswa kutathmini kama mpangilio wa mradi umeambatana na mabadiliko ya kijinsia katika mazingira maalum. Mpangilio huu wa kazi unahimiza mitazamo mitatu ya uchambuzi wa kijinsia ambayo inatathmini mabadiliko ya kitaasisi, utamaduni wa kijamii na mwenendo wa mabadiliko.



## Wanawake, Amani na Usalama

**Mtazamo wa Kitaasisi**

Taasisi za Mabadiliko

## Uanaume wenye Amani

**Mtazamo wa Utamaduni wa Jamii**

Kubadilisha Mitazamo

## Utambulisho Ingiliani

**Mtazamo wa Ubadilishaji**

Upanuzi wa Ujumuishi

# Mtazamo wa Wanawake, Amani, na Usalama

Njia hii ya kitaasisi inaangazia jinsi mgogoro na vita vinavyoathiri wanawake na wasichna kwa namna tofauti, na inatambua jukumu muhimu ambalo wanawake wanaweza na tayari wanafanya katika kujenga amani. Inakiri kwamba juhudi za amani na usalama zitadumu zaidi ikiwa wanawake ni washirika sawia katika kuzuia mgogoro wa vurugu, usambazaji wa misaada na uokoaji, na kuwemo katika kujenga amani ya kudumu.

Ushahidi kutoka kwenye utekelezaji wa Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa namba 1325 linaeleza kwamba wakati wanawake wanachangia katika michakato ya amani, mara nyingi lengo lao si kujitafutia mamlaka ila kutafuta mapatano, usitawi wa kiuchumi, elimu, na haki katika kubadilisha utawala—vyote ambavyo ni vipengele muhimu sana katika mchakato wa kupata amani ya kudumu.[9] Utafiti wa makubaliano 156 ya amani unaonyesha kwamba wakati wanawake wamejumuishwa katika michakato ya amani, makubaliano yana uwezekano wa asilimia 35 zaidi kudumu kwa angalau miaka 15.[10] mtazamo wa wanawake, amani na usalama inatafuta kuimarisha maoni haya.

Utekelezaji wa njia hizi unapaswa kujumuisha mtazamo wa kijinsia ili kuendeleza usawa wa kijinsia na kuimarisha matokeo ya mipango na sera. Mtazamo huu unawezesha wapangaji wa mipango kutambua na kushughulikia uzoefu maalum na majukumu ya wanawake na wasichana.

> Sheria ya Wanawake, Amani na Usalama ya mwaka 2017 ilitiwa saini kuwa sheria nchini Marekani mnamo Oktoba 6, 2017 (Sheria ya Umma Namba. 115-68). Inahamasisha kujumuishwa kwa wanawake na kuchangia katika michakato ya amani na usalama ili kuzuia, kukabiliana au kutatua mgogoro wa vurugu. Sheria hii inahakikisha usimamizi wa bunge kwa juhudi za serikali ya Marekani za kujumuisha mitazamo ya kijinsia katika kazi zinazohusiana na kidiplomasia, maendeleo na kazi za ulinzi katika mazingira yalliyo athiriwa na vurugu.

## Maswali ya Mwongozo:

- Je, ni kwa kiwango gani wanawake wanachangia katika michakato ya kufanya uamuzi katika familia, jamii, na/au serikali kuu?
- Je, wanawake wanachangia sawa na wanaume katika nafasi rasmi au zisizo rasmi za uongozi?
- Je, kiwango cha matukio ya vurugu za kijinsia dhidi ya wanawake na wanaume ni kiasi gani?
- Je, wanawake wanadhibiti mapato yao ya kibinafsi na/au ya familia? Je, wanawake wanaweza kurithi au kumiliki shamba au rasilimali?
- Je, uhuru wa usafiri unaonekana vipi? Je, wanawake na wasichana wanaweza kusafiri kwa uhuru mbali na desturi zao za kila siku?



## Kugeuza Nadharia kuwa Vitendo: Nigeria

Nigeria imefaulu kubadilisha jeshi lake na kuimarisha vita vyake dhidi ya kikundi hatari cha Boko Haram, lakini katika vita hivi, nchi inakabiliwa na uhamaji mkubwa na mahitaji mengi ya kibinadamu. Ilinukuliwa kwamba maarufu kwa ubadilishaji wa mamlaka wa amani, uchaguzi wa mwaka 2015 ulikuwa muhimu sana, lakini utawala wa kujumuisha kila mtu utahitaji bidii zaidi. Wajenga amani ambao wanataka kuimarisha utawala nchini Nigeria lazima wazingatie kwa makini jinsi ambavyo mamlaka hugawanywa kijinsia nafasi rasmi au zisizo rasmi za utawala. Kwa mfano, wanawake wanawakilishwa bungeni, katika mifumo ya sheria au wizara za serikali? Je, wanawake wamewakilishwa kwa kiwango gani katika nafasi hizi? Uchambuzi wa mchango wa wanawake katika vikao vya kufanya maamuzi katika nafasi mbalimbali, na pia nafasi zao katika maswala makuu, inaweza kufichua vizuizi vya miradi jumuisha ya utawala. Kama wanawake bado hawawakilishwi katika utawala rasmi, wapangaji wa miradi wangependa kupanga mchakato sambamba au mtandao unaozingatia maono ya wanawake katika nafasi rasmi.

# Mtazamo wa Uanaume wenye Amani

Njia hii ya utamaduni wa kijamii ina chunguza jinsi vurugu inavyoathiri maadili ya kiume na uzoefu wa kufanya vurugu kuwa jambo la kawaida kwa wanaume na wavulana katika kutatua matatizo.[11] Uanaume ni tabia, mitazamo na maadili ambayo jamii inatarajia kutoka kwa wanaume na wavulana. Wapiganaji wengi vitani ni wanaume, na wanatekeleza vurugu nyingi wakati wa amani. Lakini, wanaume hawakuzaliwa wakiwa na asili ya vurugu.[12] Njia hii inakiri kwamba vurugu na mgogoro wa vurugu—pamoja na vurugu la kingono na la kijinsia[13]—ziko na athari ya muda mrefu kwa wanaume na wavulana na zinapaswa kushughulikiwa.

mtazamo wa amani wa uanaume hubadilisha hali kutoka kwa mtazamo kuwa wanaume ni lazima wawe watekelezaji wa vurugu hadi kuelewa kwamba uanaume hujengwa na jamii na unaweza kujengwa kuwa wa amani. Miradi kama Mpango wa Wanaume Vijana katika mataifa ya Balkani unalenga kupanga upya maadili ya jamii kwa kufanya kazi na vijana wavulana kupitia shule, kambi za vijana za majira ya kiangazi, shule za kiufundi, na mitandao ya kijamii kuimarisha mtazamo usio wa vurugu wa mwanamume, ikiwemo kuheshimu watu wenye jinsia na utambulisho tofauti wa kijinsia. uanaume wa amani unakabiliana na hali ya kukubali vurugu kuwa sehemu ya uanaume wao na kulenga kuondoa vurugu katika mtazamo wa uanaume au uvulana. Njia hii haitafuti kufedhehesha wanaume na wavulana lakini kuleta mwangaza mpya, mtazamo wa maono ya amani ya kuelezea maana ya kuwa mwanamme.[14] Kwa mfano, njia hii itachunguza kwa nini wanaume na wavulana hawatafuti usaidizi kutoka kwa familia na marafiki wakati wakikabiliana na madhara. Wanaume na wavulana wanaelewaje kuonyesha udhaifu wao? Mitazamo mingi potovu kuhusu uanaume —kama vile ugavi wa kazi za kutoa huduma—huchangia ubaguzi wa kijinsia na kutokua na usawa. Njia hii inaimarisha uwezo wa wanaume kutetea uanaume wa amani na usawa wa kijinsia.

## Maswali ya Mwongozo:

- Je, ni matarajio gani makuu ambayo kijana wa kiume lazima atimize ili atambulike kama "mwanaume aliyekomaa" katika jamii? Je, kuna pengo kati ya matarajio na hali halisi?
- Ni jumbe gani za kijinsia zinazotumiwa kusajili wanaume katika vikundi haramu, wanamgambo, au vikundi hatari vya vurugu? Je, jumbe hizi ni tofauti na zile zinazotumiwa kuwasajili wanawake?
- Ni kwa kiwango gani ambapo mtazamo wa uanaume unahimiza kutumia vurugu? Kwa njia zipi?
- Je, vipaumbele vya wanaume ni vipi katika majadiliano? Vipaumbele hivi vinatofautiana vipi na vile vya wanawake?
- Ni kwa kiasi gani wanaume wanaunga mkono au kutounga mkono utawala wa wanawake na usawa wa kijinsia?
- Ni mbinu gani zinaweza kutumika kuwahimiza kuunga mkono kikamilifu uwezeshaji wa wanawake katika maeneo yaliyoathiriwa na vurugu?



## Kugeuza Nadharia kuwa Vitendo: Tunisia

Ubadilishaji wa kidemokrasia wa Tunisia mara nyingi husifiwa kama mafanikio ya pekee kutoka kwa mchipuko wa mageuzi ya Kiarabu ya mwaka 2011, lakini nchi hii bado inakabiliana na ukosefu mkubwa wa ajira, taasisi dhaifu, na vitisho kutoka kwa vikundi vikali haramu. Taifa hili sasa inapaswa kufanya kazi kuzuia vikundi vikali haramu ili visisajili vijana wa Tunisia. Kadiri ukosefu wa ajira unavo ongezeka, ndivyo kizazi kipya kinazidi kuwa na mtazamo wa kihafidhina. Kuuliza maswali kuhusu njia za kitamaduni za ukuwaji kuwa mtu mzima—au uanaume —kunaweza kusaidia kuelewa mbinu za usajili za vikundi haramu vya vurugu na sababu zinazowashawishi vijana kujiunga navyo. Kwa mfano, mvulana anakuwaje mwanaume? Je, kupata ajira au kuonyesha nguvu juu ya wengine kunaashiria fulani amekuwa mtu mzima? Je, vijana wadogo wa kiume hutafuta wapi mapato kama kazi hazipatikani? Uwezekano wa usuluhishaji unaweza tafuta njia mbadala ya uanaume usiotumia vurugu.

# Mtazamo wa Utambulisho Ingiliani

Njia hii ya mabadiliko inatambua kwamba utambulisho wa kijinsia unaweza kuwa na maumbo mbalimbali, na kuwa maadili na sheria za jamii zinaweza kuunda utambulisho huu. Njia hii inachukua mtazamo wa uhusiano katika jamii, na kutambua kwamba shida haziwezi kutatuliwa kwa njia moja lakini zinapaswa kutatuliwa kupitia mbinu tofauti.

Watu wote wana utambulisho wa kijinsia. Ni muhimu kuzingatia sababu kama vile umri wa mtu, hali ya ndoa, taifa, kijinsia, tabaka, ukoo, kabila, dini na uwezo unavyoathiri uzoefu wao katika jamii. Njia hii inatoa mtazamo kutoka kwenye uchambuzi wa hoja zinazoingiliana na hauwezi kueleweka ukiwa peke yake; wazo kuwa aina duni za utambulisho wa mtu huingiliana na haziwezi kufahamika zikiwa peke yake.[15] Kwa kuelewa umuhimu wa uzoefu huu tofauti, njia hii inachambua uhusiano mkubwa na vipengele vya mamlaka katika jamii na athari za kudhibiti rasilimali, mwenendo, na sababu nyengine.

Maadili ya kijamii—hususan majukumu na matarajio kutoka kwa wanaume na wanawake ambayo jamii inaona yanafaa au kupendwa—mara nyingi ni vigumu kuyabadilisha.[16] Njia hii inatafuta kuelewa bora jinsi ambavyo utambulisho tofauti wa mtu unaathiri uwezo na mamlaka yake katika hali fulani na kwa hivyo uelewa bora wa jinsi jamii inavyoweza au kutoweza kushughulikia masaibu yake. Kwa kutafuta kuelewa vipengele vya mamlaka, mtazamo wa utambulisho ingiliani unaweza kukabiliana na desturi za kijamii ambazo husababisha au kueneza ukosefu wa usawa, hususan wa kijinsia.

## Maswali ya Mwongozo:

- Je, miundo katika familia, jamii, au katika kiwango cha kitaifa inaimarisha au kukabiliana na desturi zinazochangia vurugu?
- Je, vyombo vya habari huonyesha vipi desturi na mtazamo kuhusu wanaume, wanawake, wavulana na wasichana? Je, vikundi vidogo vya kijinsia na kingono vinawakilishwa katika vyombo vya habari?
- Je, majukumu ya wanaume na wanawake yasiyo rasmi huchangia vipi vurugu?

- Je, ni nini hufanyika kwa wanawake, wanaume, na vikundi vidogo vya kingono na kijinsia ambavyo havifuati desturi za kijinsia? Je, ni vipengele gani vya ukiukwaji wa maadili vinavyokubalika au kutokubalika?
- Ni sheria na mitindo gani iliyo—rasmi na isiyo rasmi—huruhusu ubaguzi wa kijinsia au inayoweza kutumiwa kufanya ubaguzi?



## Kugeuza Nadharia kuwa Vitendo: Yukreni

Demokrasia changa ya Yukreni inakumbwa na msukosuko na mvurugo isipokuwa ikiweza kumaliza tofauti kati ya Mashariki na Magharibi, hususan tangu mwaka 2014 wakati Krimea iligawanywa na Urusi. Taifa hili limepambana kujumuisha idadi kubwa ya wakimbizi wa ndani ambao walilazimika kutoroka nyumba zao katika miaka ya hivi karibuni. Ingawa kwa mtazamo wa kwanza mtu anaweza kudhania kwamba wanaume watapata nafasi nyingi za kiuchumi na za kujiunga katika jamii zao mpya, wengi wao walipata shida ya kupata ajira tangu walipohamishwa—au kupata kazi za hadhi sawa na kazi zao za awali. Baada ya uchambuzi makini, ni muhimu kuelewa jinsi sababu kama utambulisho wa maeneo ya wanaume (Yukreni mashariki) au uwezo wa lugha ( Kirusi dhidi ya Kiyukreni) zinavyoathiri nafasi za kujijumuisha katika jamii mpya. Tofauti na hilo, nafasi nyingi za kiuchumi zinaonekana kupatikana kwa wanawake, na hata pia nafasi zaidi za kijamii za kuingia katika shule au sokoni, kwa mfano. Miradi ya kujenga amani ambayo inafanya kazi na watu hawa zinaweza kufaidika kwa kuelewa aina nyingi za utambulisho wa watu waliohamishwa na jinsi utambulisho huo unavyoathiri majukumu rasmi na yasiyo rasmi ambayo wanaume na wanawake wanayatekeleza. Miradi inaweza kufanya kazi na wanaume hususan kwa kuelewa shinikizo la ziada kutoka nje na hisia ya hatia kwa kutopigana katika mstari wa mbele kwenye vurugu za eneo la mashariki. Kushughulikia shinikizo hizi kunaweza kuangazia nafasi mpya za kujihusisha na jamii zao.

# Kuendelea Mbele na Mchakato Wa Kijinsia

Muundo wa mradi—hata kama lengo na madhumuni yake yanaangazia hususan maswala ya kijinsia au la—ni lazima iwe kawaida kuzingatia mabadiliko ya jinsia katika muktadha maalum. Njia hizi zimependekezwa kuchambua jinsia katika muktadha wa vurugu. Njia hizi zinatofautiana katika malengo yao—kutoka kwenye mtazamo mdogo kuhusu masuala mahususi kwa wanawake au wanaume hadi kwenye uchambuzi mpana wa majukumu ya kijinsia katika jamii.

Mradi unaweza kujumuisha njia moja au kadhaa. Wafanyakazi wa mradi wanaweza kuanza kwa mtazamo wa mwanamke, amani na usalama lakini baadaye kuelewa kwamba mtazamo wa utambulisho ingiliani unachangia manufaa zaidi. Wakati wa kuamua kuhusu mtazamo, ni muhimu kuangalia malengo na madhumuni ya mradi, mabadiliko ya tamaduni za kijamii katika muktadha, na faida ya ziada ambayo kila njia inaweza kuleta katika mradi. Kuna uwezekano mkubwa kwamba njia fulani zitakuwa na umuhimu zaidi kuliko njia zingine. Kudumisha amani kwa kawaida hutegemeana na muktadha.

Hakuna sheria moja tu inayoweza kuchagua mtazamo gani bora zaidi. Lakini kwa kuanza kuuliza maswali na kuchunguza mabadiliko ya jinsia kwa kutumia njia hizi, wapangaji wa miradi wataboresha muundo wao wa mradi na kuongeza uwezekano wa kufikia malengo yao.

# Maelezo:


1 Nora Dudwick na Kathleen Kuehnast, "Gender and Fragility: Ensuring a Golden Hour," Fragility Study Group Policy Brief no. 8 (Washington DC: US Institute of Peace, Novemba 2016), www.usip.org/publications/2016/11/gender-and-fragility-ensuring-golden-hour.

2 Marie Berry, "Barrier to Women's Progress After Atrocity: Evidence from Rwanda and Bosnia-Herzegovina," *Gender & Society* 31, no. 6 (2017): 830–853, doi.org/10.1177/0891243217737060

3 Fikra za kijinsia ni neno ambalo USIP inalinatumia kuelezea hali hii ya kijamii.

4 Catholic Relief Services, "Peacebuilding, Governance, Gender, Protection and Youth Assessments: A Basic Guide for Busy Practitioners," 3rd ed. (Baltimore: Catholic Relief Services, 2017), www.ics.crs.org/resource/peacebuilding-governance-and-gender-assessments-basic-guide-busy-practitioners.

5 Kathleen Kuehnast, Chantal de Jonge Oudraat, na Helga Hernes, toleo., *Women and War: Power and Protection in the 21st Century* (Washington DC: US Institute of Peace, 2011).

6 Gabrielle Bardall, "Breaking the Mold: Understanding Gender and Electoral Violence," White Paper Series (Washington DC: IFES, Disemba 2011), ifes.org/sites/default/files/gender_and_electoral_violence_2011.pdf.

7 Sean Dunne et al., "Final Report of The Carter Center Mission to Witness the 2011–2012 Parliamentary Elections in Egypt" (Atlanta: Carter Center, 2012), www.cartercenter.org/resources/pdfs/news/peace_publications/election_reports/egypt-2011-2012-final-rpt.pdf.

8 Valerie Hudson and Hilary Matfess, "In Plain Sight: The Neglected Linkage between Brideprice and Violent Conflict," *International Security* 42, no. 1 (2017): 7–40, doi.org/10.1162/ISEC_a_00289.

9 Marie O'Reilly, "Why Women? Inclusive Security and Peaceful Societies" (Washington DC: Inclusive Security, October 2015), www.inclusivesecurity.org/wp-content/uploads/2015/10/Why-Women-Brief-10.12.15.pdf.

10 Marie O'Reilly, Andrea Ó Súilleabháin, and Thania Paffenholz, "Reimagining Peacemaking: Women's Roles in Peace Processes" (New York: International Peace Institute, June 2015), www.ipinst.org/wp-content/uploads/2015/06/IPI-E-pub-Reimagining-Peacemaking-rev.pdf.

11 Joseph Vess et al., "The Other Side of Gender: Men as Critical Agents of Change," Special Report 340 (Washington DC: US Institute of Peace, December 2013), www.usip.org/publications/2013/12/other-side-gender.

12 Gary Barker et al., "Evolving Men: Initial Results from the International Men and Gender Equality Survey (IMAGES)" (Washington, DC, and Rio de Janeiro: International Center for Research on Women and Instituto Promundo, 2011), http://promundoglobal.org/wp-content/uploads/2014/12/Evolving-Men-Initial-Results-from-IMAGES.pdf.

13 Dara Kay Cohen, Amelia Hoover Green, and Elisabeth Jean Wood, "Wartime Sexual Violence: Misconceptions, Implications and Ways Forward," Special Report 323 (Washington DC: US Institute of Peace, February 2013).

14 Kimberly Theidon, "Reconstructing Masculinities: The Disarmament, Demobilization, and Reintegration of Former Combatants in Colombia" *Human Rights Quarterly* 31, no. 1 (2009): 1–34, doi.org/10.1353/hrq.0.0053.

15 Kimberle Crenshaw, "Demarginalizing the Intersection of Race and Sex: A Black Feminist Critique of Antidiscrimination Doctrine, Feminist Theory, and Antiracist Politics," University of Chicago Legal Forum 1989, no. 1, article 8, http://chicagounbound.uchicago.edu/uclf/vol1989/iss1/8.

16 Charlotte Watson, Hannah Wright, and Hesta Groenewald, "Toolkit: Gender Analysis of Conflict" (Saferworld, 2016), www.saferworld.org.uk/resources/publications/1076-gender-analysis-of-conflict.

## Nadharia na Mfumo jumuishi wa Jinsia Zote

Mwongozo wa Nadharia na Mfumo wa Kujumuisha Jinsia Zote (GIFT) ni njia rahisi na zana ya kina inayowezesha kujumuisha uchambuzi wa kijinsia katika uundaji wa mradi. Kwa sababu kazi ya kudumisha amani inategemea muktadha, GIFT inaweka mbele njia tatu za uchambuzi wa kijinsia-mtazamo wa Wanawake, Amani na Usalama; mtazamo wa Uanaume wenye Amani; na mtazamo wa Utambulisho Ingiliani-ambazo zote zinaangizia mabadiliko ya kijinsia katika mazingira fulani ili kutengeneza vyema miradi ya kudumisha amani.

## Kuhusu Taasisi Hii

Taasisi ya United States Institute of Peace ni taasisi huru ya kitaifa, iliyoanzishwa na Bunge na imejitolea kutimiza dhana kwamba dunia isiyo na mgogoro, ni jambo linalowezekana, halisi na muhimu kwa usalama wa Marekani na wa kimataifa. USIP inafuatilia maoni haya katika maeneo yenye vurugu, ikifanya kazi na washirika wa maeneo husika kuzuia vurugu kugeuka kwa umwagaji damu na kuimaliza inapotokea. Taasisi inatoa mafunzo, uchambuzi, na rasilimali nyengine kwa watu, mashirika na serikali zinazojitahidi kujenga amani.


UNITED STATES INSTITUTE OF PEACE
Making Peace Possible

2301 Constitution Avenue NW
Washington, DC 20037
202.457.1700
www.USIP.org